TANGAZO LA SERIKALI Na. 203 la tarehe 17/3/2023

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)
(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 153 (1))*

MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA (HIFADHI YA MAZINGIRA) YA HALMASHAURI YA WILAYA YA IKUNGI YA MWAKA 2023

Jina

TS Na 219 la tarehe 15/4/2022

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Marekebisho ya Sheria Ndogo ya (Hifadhi ya Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi ya Mwaka 2023, na itasomwa kwa pamoja na Sheria Ndogo ya (Hifadhi ya Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi ya Mwaka 2022 ambayo hapa imerejewa kama “Sheria Ndogo Kuu”.

Marekebisho ya Kifungu cha 3 na 4

2. Marekebisho yamefanyika katika:

(a)Kifungu cha 3 (1) (a) cha Sheria Ndogo Kuu kwa kukifuta Kifungu hicho na kupangilia upya aya ambapo iliyokuwa aya ya (b) inakuwa aya ya (a) na zinazofuata kwa mtiririko huo.

(b) Kifungu cha 4 (1) (a) cha Sheria Ndogo Kuu kwa kukifuta Kifungu hicho na kupangilia upya aya ambapo iliyokuwa aya ya (b) inakuwa aya ya (a) na zinazofuata kwa mtiririko huo.

Dodoma,
Machi, 2023

ANGELLAH JASMINE KAIRUKI (MB.),
*Waziri wa Nchi – OR- TAMISEMI*